# LEARNING BY EAR 2009
## Economics – 9th episode

## SUCCEEDING IN THE BUSINESS WORLD

| | |
|---|---|
| **Series**: | **''THE STORY OF TWO YOUNG PEOPLE, WHOSE SUCCESS STEMS FROM THEIR POCKET MONEY''** |
| **Author:** | **Frédéric GAKPARA** |
| **Editors:** | **Yann Durand and Sandrine Blanchard** |
| **Translator:** | **Anne Thomas** |
| **Kisuaheli :** | **Eric Ponda** |

**NINTH EPISODE**: **"Free fall!''**

**Characters**:
- **John** (*20-year-old CEO of AOOT*)
- **Jane** *(20-year-old, Commercial Director of AOOT)*
- **Mrs Sika** *(24 years old, Secretary AOOT)*
- **Mr Zewouze** *(26-year-old accountant at AOOT)*
- **Dad** *(Jane and John's father, 49 years old)*
- **Granma** *(Jane and John's grandmother, 70 years old)*
- **Uncle Sami** *(Jane and John's uncle, 52 years old)*
- **Envoy from Foundation of African Entrepreneurs** *(46 year-old-man)*
- **Hotel receptionist** *(Woman 50 years old)*
- **Shouts of workers on strike, Scene1**

**Learning by Ear Soundtrack**

## Intro

**NARRATOR**: Nimatumaini yangu kwamba hujambo msikilizaji mpenzi wa makala haya ya Learning by Ear yanayotayarishwa na Deutsche Welle, tukiwa bado tunazungumzia masuala ya Uchumi. Hadithi yetu inahusu Vijana Mapacha ambao kutokana na juhudi zao za kubania matumizi,kumewawezesha kufaulu katika Biashara.

Jane amerejea kutoka ziara iliyokuwa na ufanisi nchini Ujerumani na Switzerland, ambako amefanikiwa kukukutana na wateja wapya.

Lakini furaha hiyo inakatizwa ghafla anapofika ofisini na kukuta wafanyi kazi wake wote wanagoma kufanya kazi. John aliyewasili siku mbili kabla, ametoweka.! Sasa Jane yuko ofisini na mhasibu mkuu na sekretari wake kujaribu kutatua mgogoro huo.Karibu tuandamane katika kipindi cha leo.

**Scene 1, IN JANE'S OFFICE**
JANE, MRS SIKA, MR ZEWOUZE…

**ATMO**: *sound of air conditioning, employees outside striking*

**1.** **Crowd:** Bwana ..John … tunataka mishahara yetu! Bw John!

**2.** *Jane is furious. She is pacing up and down her office.*

**3.** **Jane**: Kwani hawa wafanyi kazi hawajalipwa kwa miezi mingapi?

**4.** **Mr Zewouze**: Hawajalipwa kwa miezi mitatu.. ***Madam!.***

**5.** **Jane**: Miezi mitatu? Na hizi hundi zilizoko katika meza ya Kaka John ni za nini, si ni za mshahara?

**6.** **Mrs Sika**: Ni za mshahara, ndio ziliandikwa na Bw John lakini zikakataliwa na benki kutokana na ukosefu wa pesa , na zaidi tukapewa onyo na benki.…

**7.** **Jane**: Eti nini? Kwani John amerukwa na akili ? Anaandika hundi zisizo na pesa ,hajawalipa wafanyi kazi kwa muda wa miezi mitatu,na hawezi kuniambia? Lakini wewe,ndie mhasibu au sivyo?

**8.** **Mr Zewouze**: Ndio ***Madam!***

**9.** **Jane**: Hata wewe hujalipwa kwa miezi yote hiyo

**10.** **Zewouze**: Eeee… hapana ***Madam!***

**11.** **Jane**: (*outraged*)
Oh, kumbe, wewe ndie mshirika wake munaokula pesa pamoja.! Unatoa pesa hapa na

milioni 11 na kumpelekea Brazil huku wafanyi kazi wenzake wakiwa hawajalipwa mishahara yao. Nadhani marupurupu yako ni mazuri sivyo. Bibi Sika amekuwa akipata mshahara wake?

**12. Mrs Sika**: Hapana, ***Madam!*** Yangu ni miezi miwili!.

**13. Jane**: (*angry*)
Hii ni balaa gani? Kwanini hamukunijulisha kinachoendelea? Iwapi faida ya kampuni? Kwanini tunashindwa kulipa mishahara ya wafanyi kazi kwa muda wa miezi ,ilhali tunapata faida ya milioni kumi kila wiki ? (*Shouting*) Nijibu Bw. Zewouze!

**14. Mr Zewouze**: Ni mkurugenzi ……

**15. Jane**: (*Shouting*)
Mkurugenzi nini?

**16. Mr Zewouze**: Anatumia pesa nyingi kufanya ziara za ng'ambo.Kila wakati ni safari za ng"ambo akiandamana na rafiki wake wa kike huku akidai ni ziara ya kikazi. Mara nyingine anawatuma wasichana kuja kuchukua pesa hapa ofisini. Na pesa zote hizo zinaishia Klabu.

**17. Jane**: (*Horrified*)
Hiyo ndio imefilisha kampuni hii ambayo inapata kima cha faranga milioni 500 kila mwaka?

**18. Mr Zewouze**: Hutumia kiasi kikubwa cha pesa Casino. Mbali na hayo hivi majuzi pia amepoteza pesa nyingi katika mradi wa Kahawa nchini Brazil ambao haukufaulu.

**19. Jane**: Amepoteza kiasi gani?

**20. Mr Zewouze**: Casino , sijui alipoteza ngapi lakini katika mradi huo wa Kahawa nchini Brazil alipoteza kiasi cha faranga milioni 260

**21.**

**22. Jane**: (*Shouting*) Nini????

**23. ATMO**: *Silence. We can hear the shouts from the demonstrators outside.*

**24. Jane**: Alidhania tu au ni kuhadaiwa? Hii ndio sababu hajakanyaga nyumbani tangu arejee nchini. Yuko wapi sasa? (*She shouts*)Nakuuliza Bw, Mr. Zewouze! Yuko wapi kaka yangu???

**25. Mr Zewouze**: Yuko Grand Hotel.

**26. Jane**: Chumba nambari ngapi?

**27. Mr Zewouze**: (*mumbles*)
36.

**28. ATMO:** *sound of Jane running and slamming the door*

**NARRATOR**: Jane achukua funguo za gari lake na kuondoka haraka kuelekea Hotelini anamoishi Kaka yake.

**Scene 2, AT THE HOTEL**
JANE, RECEPTIONIST, JOHN…

**29. ATMO:** *Jane runs up the stairs to the hotel*

**30. Jane**: (*out of breath and angry*)
Habari, namtafuta Bw John , chumba nambari 36.

**31. Receptionist**: Anakutarajia?

**32. Jane**: Mimi ni Dada yake. Sihitaji kibali kumuona!

**33. Receptionist**: Nadhani yuko pale anaogelea.

**34. ATMO**: *By the swimming pool, clients splash each other.*

**35. Jane**: (*she calls, still angry*)
Habari , John!

**36. John**: (*surprised*)
Nani aliyekueleza niko hapa?

**37. Jane**: (*fuming*)
Usinichezee John? Yaani huoni aibu, wewe unastarehe hapa hotelini na kule kampuni yetu inaporomoka kwa sababu yako, na unaniuliza bila ya kukosa aibu nani aliyeniambia uko hapa? Unajua kwamba wafanyi kazi wetu wanagoma?

**38. John**: (*mocking*)
Nitawafuta kazi.

**39. Jane**: Oh, kumbe? Ni rahisi hivyo? Ni vipi utawalipa mishahara na marupurupu yao? Nimeona zaidi ya hundi 20 kwenye meza yako.Kwani umeshikwa na wazimu John.Ulienda Dubai kupoteza pesa tu kwenye Casino kisha ukaelekea Brazil ambako ulihadaiwa kiasi cha milioni 260 kwa mradi wa Kahawa ambao haukufaulu! Na hujasema lolote tangu wakati huo.? Kusema kweli umeniabisha sana John!

**40. John**: Nani aliyekwabia yote haya? Ni Zewouze? (*threatening*) Sitaki kumuona tena katika ofisi hiyo..

**41. Jane**: Kwani wewe ni nani? Yaani umesahau haraka hivi mahali ulikotoka? Umesahau tumekuwa tukizunguka katika barabara za mji huu na teo vichwani tukiuza Njugu? Na unasahau kwamba hizo ni pesa zangu pia? Si pesa zako peke yako!

**42. John**: Usijali nitakulipa!

**43. Jane**: Vipi? Kwa kuwahadaa wasichana? Unawazimu!

**44. John**: Wacha kuongea na mimi hivyo…

**45. Jane**: Utanifanya nini John? Au utanipiga? Nipige basi! Nakuonea huruma sana John!

**46. John**: Unanionea Huruma na mbona sioni ukilia?

**47. Jane**: (*cold*)
Najuta kwanini nikakubali akaunti yetu ifunguliwe kwa jina lako. Umenitoa imani kabisa John.Siwezi kukuamini tena.Lakini kumbuka utajuta kwa upuzi unaofanya!. Kila la kheri!

**48. ATMO**: *Jane leaves. She walks down the steps of the hotel. Sound of door. She starts the car and drives off fast. All of a sudden the car swerves, she tries to break desperately and then crashes against an electric pole. Passers-by shout. Ambulance sirens …*

**NARRATOR**: Jane anazimia na kupelekwa moja kwa moja hospitalini akiwa hali mahututi. Baada ya siku 11 akiwa hali mahututi , Jane sasa anaruhusiwa kuonana na wageni .Babake,Bibi na baba mdogo Sami kutoka Zurich amefika Hospitalini kumuona

**Scene 3, AT THE HOSPITAL**
JANE, DAD, GRANMA, UNCLE SAMI, EMCI…

**49. ATMO**: *African hospital. Patients groan, cry, sound of stretchers.*

**50. Granma**: (*Crying to herself*)
Kuna nini, ni kitu gain kilichompata malaika wangu? Ohh .. Ohh..Mjukuu wangu, umefufuka….! .au amerogwa, nani anayetaka kukuua mjukuu wangu Jane?

**51. Uncle Sami**: Bibi ukiendelea kulia, hatutaruhusiwa tena hapa Hopsitalini!

| | | |
|---|---|---|
| **52.** | **Granma**: | (*Listening to nobody*)<br>Malaika wangul. Ukifa nitazikwa na nani mimi? |
| **53.** | **Dad**: | Bibi,nyamaza!... usilie Nyamaza tafadhali…, Jane hayumo tena hatarini.hayuko katika hali mbaya sana. |
| **54.** | **Jane**: | (*Weakly*)<br>Bibi,.. usilie… |
| **55.** | **Uncle Sami**: | Jane, sote tuko hapa!.Utatoka hospitalini hivi karibuni. Tuliambiwa yote yaliyotokea.Kampuni itakuwa sawa hivi karibuni. Nitatafuta mkopo kulipa madeni yote na kufidia hasara ya kufutilia mbali mauzo yenu katika soko la nje |
| **56.** | **Jane**: | John yuko wapi? |
| **57.** | **Dad**: | Ameenda nyumbani, alikua hapa sasa hivi kabla wewe kupata fahamu. |
| **58.** | **Jane**: | (*weak still, until the end of the scene*)<br>Nilimuona kwa mbali nilipokuwa bado katika hali hiyo. Kuna watu walikuwa wananisukuma kuelekea shimo jeusi. Na John alikuwa amenishikilia nisianguke.Pia marehemu Mama alikuwepo akiwa amevalia mavazi meupe na |

akaweza kuwafukuza watu hao. Alitabasamu kisha akatoweka.

**59. Dad**: Siku hizi John hatoki tena nyumbani.Amekonda sana siku hizi. Najua sasa anajutia yote aliyotenda.

**60. Uncle Sami**: Ajute asijute, mimi nimechukua vitabu vyote vya hundi, na kufunga akaunti zake zote. Pia nimemwambia asikanyage tena katika ofisini hadi tutakapojadiliana mambo fulani.

**61. Jane**: Bado nina pesa kwenye akaunti yangu. Kama bado kunamatatizo ya kuwalipa wadeni wake unaweza kutumia pesa hizo his debts.

**62. Granma**: Ungependa nikuletee chochote mjukuu wangu?

**63. Jane**: Usijali , nadhani kuna kila kitu hapa

**64. ATMO**: *Light knocks at the door, which opens slowly.*

**65. Dad and Uncle Sami**:

Karibu!

**66. Foundation envoy**: Asanteni sana ! Habari za jioni!

**67. Granma**: Nzuri!

**68. Foundation envoy**: Nimetoka shirika la wafanyi biashara Barani Africa.Tumepata habari kuhusu ajali iliyompata Bi Jane. Shirika letu linatoa pole na kuungana na familia kumuombea Jane afueni ya haraka!..

**69. Jane**: Asante sana, Huyu ni Babangu, baba mdogo na huyu ni Bibi.

**70. Foundation envoy**: Nimefurahi kuwajua. Shirika limeamua kugharimia deni la Hospitali.

**71. Dad**: (*surprised*)
Tumeshukuru sana. Tutakuja kwenye ofisi zetu Jane atakapopata nafuu.

**72. Foundation envoy**: Rais wa shirikisho letu pia amenigusia kwamba kampuni inakabiliwa na hali ngumu ya kifedha.Kwa kuzingatia hali ilivyo ya ukosefu wa kazi nchini, itakuwa aibu kwa kuiacha kampuni hiyo ifilisike kwani imetoa ajira kwa zaidi ya watu 300.Hatungependa juhudi za vijana hawa ziangamie bure ,na rais wa shirikisho amekubali kutoa kiasi cha faranga milioni 350 kupiga jeki kampuni hiyo.Na tunatumaini kuwa usimamizi wa kampuni utawajibika siku zijazo.

**73. Uncle Sami**: Tunawashukuru sana kwa msaada wenu.Asanteni sana .Na ninawahakikishia kuwa wanabiashara hawa chipukizi wamepata funzo!

**74. Foundation envoy**: Na kabla sijenda hapa kunamualiko wa kampuni hiyo kuliwakilisha Bara la Africa wakati wa maonyesho ya kimataifa ya biashara yatakayoandalia nchini Canada.Utakuwa miongoni mwa ujumbe wetu utakaohudhuria maonyesho hayo miezi minne ijayo.

**75. ATMO**: *thank you from the whole family.*

**<u>Outro</u>**

**NARRATOR**: Ni kwa habari hizo njema ndipo tunapofika mwisho wa makala haya ya tisa kuhusu masuala ya Biashara na Uchumi. Pesa zilimfanya John akapagawa na kujiingiza katika vitendo viovu na hatimaye kuifilisisha biashara yao.Hali ambayo nusra igharimu maisha ya Jane.Lakini kutokna na sifa, heshima na juhudi zake ameweza kuiokoa biashara hiyo

.

**76. Closing soundtrack to be left running after the outro and brought up**

**NARRATOR:** **Je** wanabishara hawa shupavu wataelekea Canada kwa maonyesho ya kimataifa? Nini kitakachotokea katika maonyesho hayo ya bishara. Ungana nasi katika makala ya 10 na ya mwisho kuhusu masuala ya Uchumi ujue yatakayojiri. Kumbuka pia unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki au kutuma maoni yako kupitia mtandao wetu wa **dw-world.de/l b e.**

Hadi wakati mwengine tutakapokutana nawe tena kwaheri kwa sasa.!

**Music up**

END